**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA CHAMWINO**

SHULE YA SEKONDARI MANCHALI WASICHANA
S. L. P. 1126, DODOMA.

Mpendwa Mwanafunzi:- ……………………………………………………….. ……………………
Anwani: c/o ……………………………......(Mzazi/ Mlezi), S. L. P……………………………………

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA MANCHALI KATIKA HALMASHAURI YA CHAMWINO MWAKA 2026

1. **PONGEZI NA KARIBU:** Kwa niaba ya jamii nzima ya Shule ya Sekondari ya Wasichana Manchali, nakupongeza sana kwa kuchaguliwa kujiunga na shule yetu, kwa pamoja tunakukaribisha sana. Yafuatayo ni maagizo ya kujiunga na shule hii.

2. **MAELEKEZO YA KUFIKA SHULENI:**

Shule hii inapatikana katika kata ya **Manchali, Wilaya ya Chamwino,** Mkoa wa Dodoma . Kwa wale wanaotokea mikoani na kushukia Dodoma mjini usafiri wa kufika Manchali unapatikana stendi ya daladala ya Nanenane (Soko la Ndugai) au kituo cha basi kilichopo Chuo cha Biashara (CBE). Baada ya kushuka utapanda gari lolote linaloelekea Kongwa, Kibaigwa, au Gairo na utashukia kituo cha Manchali. Nauli kutoka nanenane (Soko la Ndugai) ni kati ya shilingi 5,000/= na 6,000/= .

Kwa anayetokea barabara ya Morogoro naye atashukia kituo cha Manchali (ni kabla ya kufika Dodoma mjini hivyo amjulishe kondakta mapema). Kutoka kituo cha mabasi cha Manchali hadi shule ilipo ni kilomita mbili tu. Nauli ya pikipiki hadi shuleni ni sh. 2,000/=

3. **SIKU YA KUFUNGUA SHULE:** Shule itafunguliwa tarehe **12/01/2026** mwanafunzi unatakiwa kuripoti shuleni kati ya tarehe **12/01/2026** hadi tarehe **19/01/2026** bila kukosa. Ukishindwa kufika baada ya wiki mbili utapoteza nafasi yako bila ridhaa yako. Endapo utashindwa kuripoti ndani ya kipindi hicho nafasi yako itachukuliwa na mwanafunzi mwingine. Njoo na barua hii kwa utambulisho. Ukifika shuleni omba kuonana na mwalimu wa zamu ambaye atakupokea na

kukuelekeza kwa mwalimu wa bweni (boarding mistress) wa shule kwa ajili ya kukabidhi vifaa vilivyoelekezwa hapa chini.

4. **MAHITAJI MUHIMU YA SHULE:**

**A: SARE ZA SHULE** :-

(i) Mashati 2 meupe yenye mikono mifupi na mfuko upande wa kushoto.

(ii) Sketi 2 vazi rasmi la darasani drafti yenye rangi ya maziwa na dark bluu( sampuli ya kitambaa imebandikwa). Sketi iwe na marinda mawili kushoto na kulia, na moja kubwa katikati ( Rinda box) **na iwe ndefu kufikia kifundo cha miguu. (Karibu na unyayo).** Zinapatikana shuleni kwa atakaehitaji kwa gharama ya Shilingi 36,000/= kwa kila sketi.

(iii) T-sheti 2 ( Flana) vazi la nje ya darasa yenye rangi ya kijivu iliyoiva yenye kola, kwa watakaopenda inapatikana shuleni kwa gharama ya shilingi 10,000/= kwa kila moja.

(iv) Sweta 1 rangi ya bluu iliyoiva (dark blue) lenye shingo yenye alama "V" mbele.

(v) Tai ndefu inayoendana na rangi ya sketi. Zinapatikana shuleni.

(vi) Soksi nyeupe ndefu zisiwe na weusi kwenye unyayo angalau jozi 2

(vii) Viatu vya shule vya ngozi vyeusi vya kufunga na kamba jozi 2, kiwi na brashi yake

(viii) Nguo za nje ya darasa ( shamba dress) ambazo ni sketi 02 rangi ya kahawia, kwa watakaopenda zinapatikana shuleni kwa gharama ya shilingi 30,000/=kila sketi. **Na iwe na urefu kufikia kifundo cha miguu. (Karibu na unyayo).**

**N.B. <u>VAZI LA HIJABU</u>: - Pamoja na maelekezo (i) – (viii) vazi la Hijabu linaruhusiwa kwa kuzingatia:-**

(i) Hijabu nyeupe ya darasani.

(ii) Hijabu ya nje ya darasa rangi ya kijivu iliyoiva.

<u>B : VIFAA VINGINE :-</u>

i. Madaftari makubwa (counter books) kumi (10)
ii. Kalamu ya wino (pen,) penseli na rula.
iii. Mkebe kwa ajili ya masomo ya sayansi.
iv. Kamusi ya kingereza (Dictionary).
v. Bunda mbili za karatasi (Ream) – Moja kila mhula
vi. Ndoo mbili (lita 10).
vii. Fagio Moja la ndani (soft broom), chelewa Moja (hard broom) na moper 01, skuizer 01.
viii. Jembe moja lenye mpini mrefu na Fyekeo moja.
ix. Godoro ukubwa wa 3x6 **(ZINGATIA SIZE YA GODORO)** lenye foronya na mto mmoja.
x. Shuka mbili, rangi ya pinki.
xi. Chandarua nyeupe yenye ukubwa wa 3½

**N.B. Rimu , counterbooks, kalamu na mikebe vinapatiana shuleni kwa watakaopenda.**

C: VIFAA VYA MICHEZO

.

i. Tracksuit moja ya dark blue yenye nembo ya shule.
ii. Raba nyeupe jozi moja na soksi nyeupe kwa ajili ya michezo.

D: MAHITAJI MENGINE

i. Vyombo vya chakula: Sahani bakuli,kikombe (aina ya mfupa) kijiko na chupa ya maji ya kunywa.
ii. Nguo za ndani za kutosha, taulo za kike, sabuni za kuogea na kufulia, miswaki na dawa ya meno, mafuta ya kupaka ya mgando.

    **ZANGATIA, Perfume, spray na mafuta yenye harufu kali na yenye kemikali hayatakiwi kabisa.**
iii. Kitenge au khanga pamoja na taulo, blanketi zito.
iv. Sanduku imara (trunker)
v. Fedha kwa ajili ya matumizi binafsi isiyozidi elfu 50,000/=, zitakabidhiwa kwa mwalimu husika pindi mwanafunzi anaporipoti.
vi. Mwanafunzi aje na bima ya afya.
vii. Passport size 02
viii. Fedha ya kitambulisho shilingi 5,000/= na nembo ya shule 5,000/=

**Pamoja na maagizo haya naambatanisha nyaraka zifuatazo :-**

i. Kanuni za shule.
ii. Fomu ya hospitali
iii. Fomu ya kukubali nafasi.
iv. Fomu ya kiapo cha mzazi

5 : KANUNI MUHIMU ZA SHULE.

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu na. 25 ya Mwaka 1978. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara yenye dhamana ya Elimu Nchini, unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo:-

i. Heshima kwa viongozi, Walimu, Wazazi, Wanafunzi wenzako, na jamii kwa ujumla ni lazima.
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule ni lazima.
iii. Lugha ya mawasiliano shuleni ni kiingereza.
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa

v. Kutunza usafi wa mwili na mazingira ya shule.

vi. Mwanafunzi anatakiwa Kuvaa sare ya shule wakati wote unapokuwa shuleni na anaposafiri kwenda nyumbani na kurudi.

vii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote na kutii wito wa kengele zote, ratiba ya siku, dharura na kuwahi mahala anapohitajika mara moja.

viii. Chakula na vinywaji vitaliwa bwaloni kwa kufuata sheria za bwalo ambazo ni.

a. Hairuhusiwi kuingia na kanga au ndala bwaloni.
b. Hairuhusiwi kuingia bwaloni wakati chakula kinapoingizwa bwaloni.
c. Hairuhusiwi kupiga kelele bwaloni.
d. Vyombo vyote vya chakula vitahifadhiwa bwaloni.

ix. Hairuhusiwi kuingia jikoni isipokuwa kwa ruhusa maalumu.

x. Hairuhusiwi mwanafunzi kununua aina yeyote ya chakula nje ya shule kama matunda, maandazi, hii ni kwa ajili ya afya na usalama wa mwanafunzi shuleni.

xi. Mwanafunzi haruhusiwi kwenda vilabu vya pombe mtaani, nyumba za starehe.

xii. Hairuhusiwi kupeleka chakula darasani, bwenini isipokuwa kwa ruhusa maalumu.

xiii. Hakuna chakula maalumu (special diet) kinachotolewa kwa mwanafunzi yeyote.

xiv. Hifadhi ya chakula kwa ajili ya wachelewaji haipo, isipokuwa kwa sababu maalumu.

xv. Mzazi/mlezi/ndugu haruhusiwi kuingia na chakula au kutuma chakula au kinywaji cha aina yoyote kwa ajili ya mwanafunzi shuleni.

xvi. Kila mwanafunzi anatakiwa kuwa safi na nadhifu wakati wote.

xvii. Mwanafunzi hataruhusiwa kurudi nyumbani kwa sababu ya ugonjwa au kifo cha ndugu isipokuwa **kwa baba, mama, mlezi, kaka na dada wa kuzaliwa naye.**

xviii. Hairuhusiwi mwanafunzi kuongea na mgeni yeyote bila idhini ya uongozi wa shule.

xix. Hairuhusiwi Mzazi/ Mlezi kumtembelea mwanafunzi Kwani kila baada ya miezi mitatu wanafunzi wanarudi nyumbani.

## 4.2: MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE:

i. Wizi
ii. Uasherati na ushoga
iii. Ubakaji
iv. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile bangi, cocaine, mirungi, kuberi n.k
v. Kupigana au kupiga.
vi. Kuharibu kwa makusudi mali ya Umma.
vii. Kudharau bendera na wimbo waTaifa
viii. Kuolewa.
ix. Kupata mimba.

x. Kutoa mimba.

xi. Kugoma, kuchochea au kuongoza vurugu dhidi ya amani na usalama wa shule au watu.

xii. Kukataa adhabu kwa makusudi.

xiii. Mwanafunzi kuwa na simu ya mkononi.

xiv. Kukosa kufika shuleni kwa siku 90 mfululizo bila taarifa rasmi.

5.0 Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

KARIBU SANA KATIKA SHULE HII.

REDINADA. P. BIRYAMUTWE

MKUU WA SHULE.

TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO, USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO:-

MKUU WA SHULE. 0753355580/0617 057580

MAKAMU MKUU WA SHULE

Mwl Severine William Msekaa 0757579755

MWANDAMIZI TAALUMA.

Mwl Gaitani Noel Kudenya. 0787806447

MALEZI,

Mwl Agness Nelson Mwaitete 0759878907

OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA WILAYA YA CHAMWINO

SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA MANCHALI

FOMU YA KUKUBALI KUJIUNGA NA SHULE

A: SEHEMU YA MWANAFUNZI

1.Mimi (majina kamili matatu)……..........................................................................

Nimekubali kuingia kidato cha..............katika shule ya Sekondari ya Wasichana Manchali kuanzia tarehe........................hadi nitakapomaliza kidato cha............

2. Naahidi kuwa, nitatii sheria na kanuni zote za Shule na kushiriki katika shughuli zote za Shule kikamilifu kulingana na ratiba ya Shule.

3. Tarehe ya kuzaliwa..................................
Kijiji...........................Kata..............................Wilaya..................................

Sahihi ya mwanafunzi..................................Tarehe........................

Namba ya simu ya Mzazi / Mlezi.....................................................

**OFISI YA RAIS.**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA. HALMASHAURI YA WILAYA YA CHAMWINO.**

**SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA MANCHALI.**

**KIAPO CHA MZAZI/MLEZI (**kata isiyohusika)

PASSPORT SIZE

1. Mimi (majina kamili) …………………………………………………………………
   Simu.................................. ninakubali mtoto wangu asome katika shule ya sekondari ya Wasichana Manchali kwa muda wote atakaopaswa kuwa hapo kimasomo.
2. Kazi ya baba..........................................................................................................
3. Jina kamili la mama.................................................. Simu ……..............................
4. Kazi ya mama ..........................................................................................................
5. Anwani ya mzazi/mlezi.........................................................................................
6. Wafuatao ni ndugu zake ninaowatambua wanaweza kumsaidia wakati wa dharura:

| | Jina kamili | Mahusiano | Anakoishi | Simu |
|---|---|---|---|---|
| i. | ..................................... | ......................... | ........................ | ................. |
| ii. | ..................................... | ......................... | ........................ | ................. |

7. Dhehebu la dini ya mtoto ni ...............................................................

8. Ripoti za maendeleo ya mwanafunzi ziwe zinatumwa kwa:

..................................................................................................

..................................................................................................

..................................................................................................

**1. JINA LA MZAZI/ MLEZI ……………………………………………………….**

**NAMBA YA SIMU ……………………………**

**SAINI ………………………………………..**

**TAREHE …………………………………….**

# MANCHALI GIRLS SECONDARY SCHOOL

## MEDICAL EXAMINATION FORM

To be completed by Medical Officer incharge in respect of all form I- IV entrants

Full name ………………………….. Age ……………………………… Sex …………………….

Year ……………………….

1. Blood count (red and white) ………………………………. 2. Urine analysis Test ……………………………………………
3. Syphilis Test ……………………………………………..
4. T.B Test ……………………………………………………….
5. Eye Test ……………………………………………………….
6. Ears ……………………………………………………………
7. Spleen …………………………………………………….
8. Abdomen …………………………………………………

ADDITIONAL INFORMATION

E.g.: Physical defects or impairment (s) Infections Chronic or family diseases etc.

…………………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………………………
…………….

……………………………………… ……………………………………….. NAME AND DESIGNATION

SIGNATURE AND OFFICIAL STAMP

………………………………………….. ……….……………………………

STATION DATE

NOTE

Medical officer during the course of this examination, please attend the individual according to any diagnosed case.

**NB:** This form should be sent to school with acceptance form or brought when you come to school. No student is enrolled without certification of physical fitness.